**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE**

Tarehe: 17/01/2022

# TANGAZO LA AJIRA YA MKATABA YA KAZI ZA UFUNDI KWA AJILI YA UJENZI WA JENGO LA WAGONJWA WA DHARURA (EMERGENCY MEDICAL DEPARTMENT) NA NYUMBA YA WATUMISHI (THREE IN ONE) KATIKA KITUO CHA AFYA KYIMO

## ZABUNI NA. LGA/071/2021/2022/RDC/W/28 LOT I & II

1. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe anawatangazia wananchi wote kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe imepokea fedha kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Wagonjwa wa dharula (EMD) katika Hospitali ya Wilaya Tukuyu na Ujenzi wa Nyumba za Watumishi (Three in One).
2. Hivyo basi, Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya inakaribisha kazi za Mikataba ya Muda Mfupi za Mafundi wenye sifa na uzoefu katika shughuli za Ujenzi ambao utafanyika kwa njia ya Manunuzi ya "Force Account" kwa majengo yafuatayo:-

| Lot Na. | Jina la Mradi | Kazi kuu zitakazofanyika |
|---|---|---|
| I | Ujenzi wa jengo la Wagonjwa wa dharula (EMD) katika Hospitali ya Wilaya Tukuyu | Ufundi Uashi, Uchomeleaji wa vyuma, kusuka nondo, usuukaji na ufungaji wa mifumo ya umeme na TEHAMA (ICT), Mifumo ya maji safi na taka, upigaji rangi, uwekaji marumaru na terrazzo kwa baadhi ya sehemu za ndani ya jengo n.k |
| II | Ujenzi wa Nyumba za Watumishi (Three in One) | Ufundi Uashi, usuukaji na ufungaji wa mifumo ya umeme una Mifumo ya maji safi na taka, upigaji rangi, uwekaji marumaru n.k |

3. Hivyo basi, wanahitajika mafundi ujenzi wenye sifa katika fani zifuatazo:-

   i. **Fundi Uashi**
      - Awe na elimu ya ufundi Uashi/ujenzi na mwenye kujua kusoma ramani za majengo

- Awe na mafundi wasaidizi wenye ujuzi wa kujenga, kusuka nondo (kwa jengo la EMD), usukaji wa mifumo ya umeme, maji safi na taka, kupiga rangi na kuweka marumaru kwenye sakafu na ukutani. Awe na fundi wa kuweka terazo kwenye baadhi ya sehemu za ndani ya jengo(kwa jengo la EMD).

ii. **Fundi Aluminium**
- Awe na uwezo wa kusoma michoro na vipimo vya ramani.
- Awe na uwezo wa kutengeneza madirisha ya Aluminium na milango ya alco bond).
- Awe amewahi kufanya kazi ya ujenzi katika majengo ya Serikali au kwenye makampuni.

iii. **Fundi Seremala** (inahusisha utengenezaji wa milango na fremu za milango).

- Awe na uwezo wa kutengeneza milango ya mbao ngumu
- Awe amewahi kufanya kazi ya ujenzi katika majengo ya Serikali au kwenye makampuni.

iv. **Fundi kuchomelea vyuma** (ambao utajumuisha kutengeneza magrill ya milango na madirisha).
- Awe na uwezo wa kutengeneza milango ya "grill"
- Awe amewahi kufanya kazi ya ujenzi katika majengo ya Serikali au kwenye makampuni.

v. **Fundi wa Mifumo ya TEHAMA**
- Awe na uwezo wa kutengeneza mifumo mbalimbali ya TEHAMA (ICT)
- Awe amewahi kufanya kazi ya ujenzi katika majengo ya Serikali au kwenye makampuni(kwa jengo la EMD).

**Sifa za ziada za muombaji**

i. Awe Mtanzania mwenye umri kuanzia miaka 18 na kuendelea
ii. Awe na Namba ya Utambulisho wa Ulipaji Kodi (TIN)
iii. Awe na akaunti kwenye benki yeyote iliyopo ndani ya Rungwe
iv. Awe na uzoefu wa kufanya kazi za ujenzi za serikali na mwenye uelewa na taratibu zake. Aambatanishe nyaraka muhimu ili kuthibitisha uzoefu wake katika kufanya kazi za Serikali (yaani aambatanishe nakala za barua za tuzo za kazi alizowahi kufanya, nakala za mikataba ya kazi za

ujenzi, nakala za Hati za Malipo za kuanzia mwaka 2018 hadi mwaka 2022).

v. Mwombaji awe na uwezo wa kifedha (Mtaji) wa kuwalipa mafundi wake wasaidizi pasipo kuomba kulipwa malipo ya awali (Advance Payments); na kwa msingi huo aambatanishe na taarifa za kibenki (Bank Statement) angalau ya mwaka mmoja (1).

vi. Awe mzalendo na mwenye kujituma katika kazi.

vii. Awe na Elimu angalau cheti cha ufundi

**Aidha, pia Mwombaji anapaswa kuzingatia masharti yafuatayo:-**

a) Mwombaji lazima aandike barua ya maombi kwa jina lake binafsi au kwa jina la biashara akiainisha kazi anayokusudia kufanya.

b) Mwombaji aambatanishe barua ya utambulisho kutoka ofisi ya Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa.

c) Mafundi watakaobahatika kupata kazi watalazimika kuajiri mafundi wasiopungua 6 wenye uwezo na uzoefu, wasaidizi wa kutosha kwa kadri ya ukubwa wa kazi husika.

d) Awe tayari kufanya kazi muda wote kwa mujibu wa masharti ya mkataba utakaoandaliwa bila visingizio.

4. Barua za maombi zikiwa zimeambatanishwa na nyaraka tajwa hapo juu katika upande wa sifa na masharti ziwawasilishwe ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya, Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, S.L.P 148, Tukuyu yakiwa yamefungwa vizuri kwenye bahasha nyuma ya bahasha ikitaja jina la kazi inayoombwa.
5. Mwisho wa kupokea maombi ya kazi tajwa hapo juu ni tarehe 24/01/2022 saa 4:00 Asubuhi. Aidha, maombi yatakayoletwa baada ya hapo hayatakubaliwa.
6. Waombaji wote wanatakiwa kuhudhuria usaili wa mafundi/kampuni utakaofanyika tarehe 24/01/2021 saa 5:00 asubuhi tafadhali zingatieni muda huu.

7. Wako katika Ujenzi wa Taifa,

Mchau, R.B
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE**

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
RUNGWE